

WARAKA MFUPI WA KIBALI CHA MAANDISHI KWA  
WASHIRIKA WASIOZUNGUMZA KIINGEREZA

**LAZIMA WARAKA HUU UANDIKWE KWA LUGHA AMBAYO MSHIRIKI ANAELEWA**

**Kibali cha Kushiriki katika Utafiti**

Unaombwa kushiriki katika utafiti. Kabla hujaamua, lazima kwanza mchunguzi akupe taarifa ili kukusaidia kuelewa kile ambacho huenda ukahitaji ili kushiriki utafiti na sababu ya KUTOTAKA kushiriki katika utafiti.

Lazima mchunguzi akuambie kuhusu madhumuni, taratibu na muda wa utafiti, taratibu zozote ambazo zinaweza kuwa za majaribio, hatari zozote zinazoweza kutabirika, maumivu, manufaa ya utafiti, upasuaji au tiba zozote mbadala zenye manufaa na jinsi usiri utakavyodumishwa.

**[Ikiwa utafiti huu unahusu mkusanyiko wa taarifa ya kutambulisha au sampuli, jumuisha yafuatayo:]**

Mchunguzi pia atakuambia ikiwa na jinsi taarifa yako **[na/au sampuli]** inavyoweza kutumiwa siku zijazo au kushirikiwa na wachunguzi wengine.

Inapowezekana, lazima pia mchunguzi akuambie kuhusu fidia au tiba yoyote inayopatikana majeraha yakitokea, uwezekano wa hatari zisizotabirika, hali wakati mchunguzi anaweza kusimamisha ushiriki wako, gharama zozote za ziada, kinachotendeka ukiamua kuacha kushiriki, utakapoambiwa kuhusu matokeo mapya yanayoweza kuathiri utayari wako wa kushiriki, idadi ya watu katika utafiti na taarifa kuhusu jinsi sampuli zitakavyotumiwa na kitakachotendeka taarifa iliyotolewa kwenye sampuli.

Ikiwa una maswali kuhusu utafiti au ukihisi umejeruhiwa, unaweza kuwasiliana na:

Jina:

Simu:

Ikiwa una maswali, matatizo au malalamishi kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Ulinzi wa Utafiti wa Binadamu (Human Research Protection Office), kwa nambari 1-(800)-438-0445 au barua pepe [hrpo@wusm.wustl.edu](mailto:hrpo@wusm.wustl.edu).

Ushiriki wako katika utafiti huu ni wa hiari na hutaadhibiwa wala kupoteza manufaa ukikataa kushiriki wala kuamua kuacha kushiriki.

Maelezo ya jaribio la kimatibabu yatapatikana kwenye <http://www.ClinicalTrials.gov>, kama inavyohitajika na Sheria ya Marekani. Tovuti hii haitajumuisha taarifa inavyoweza kukutambulisha. Tovuti itajumuisha muhtasari wa matokeo mara chache. Unaweza kutafuta Tovuti hii wakati wowote.

Ukikubali kushiriki, lazima upewe nakala ya waraka huu iliyotiwa sahihi na yenye tarehe ambayo imeandikwa kwa lugha unayoelewa na nakala ya waraka wa muhtasari wa maandishi ya Kiingereza (kibali).

Kutia sahihi waraka huu kunamaanisha kuwa umesomewa **taarifa** zote kutoka kwenye waraka wa muhtasari wa Kiingereza (kibali), kuwa mmejadili taarifa yako na maswali yako kujibiwa na kwamba unakubali kushiriki kwa hiari.

\_\_\_\_\_  
Jina la Mshiriki Lililochapishwa

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Mshiriki

\_\_\_\_\_  
Tarehe

\_\_\_\_\_  
Jina la Shahidi Lililochapishwa

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Shahidi

\_\_\_\_\_  
Tarehe

*Mshiriki:*

*Tia Sahihi Fomu hii Fupi PEKEE*

*Shahidi:*

*Tia Sahihi Fomu hii Fupi na Muhtasari wa Kiingereza (Waraka wa Kibali)*

*Mtu Anayechukua Kibali:*

*Tia Sahihi Muhtasari wa Kiingereza PEKEE (Waraka wa Kibali)*